**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**BARAZA LA TAIFA LA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI (NEEC)**

# MWONGOZO WA UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA TAIFA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI (NMSFEE)

**FEBRUARI, 2016**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**BARAZA LA TAIFA LA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI (NEEC)**

# MWONGOZO WA UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA TAIFA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI (NMSFEE)

**FEBRUARI, 2016**

# YALIYOMO

**KAULI YA WAZIRI MKUU WA JAMHURI WA MUUNGANO WA TANZANIA........................................................................................iii**

**DIBAJI........................................................................................................iv**

**SURA YA KWANZA ..................................................................... 1**

1.0 UTANGULIZI.........................................................................................1

1.1 Madhumuni ya mwongozo ..............................................................2

1.2 Misingi ya Utekelezaji wa Mwongozo ..............................................2

**SURA YA PILI ............................................................................... 4**

2.0 MKAKATI WA TAIFA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI. ........4

2.1 Nguzo za Mkakati wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi............4

2.1.1: Kukuza Uchumi na Kujenga Mazingira ya Uwekezaji...........................4

2.1.2: Uboreshaji wa Mfumo wa Utozaji Kodi, Sheria, Kanuni, Leseni na Huduma Nyingine za Serikali.............................................................5

2.1.3: Kukuza Mitaji..........................................................................................6

2.1.4: Kuinua Viwango vya Elimu Na Ujuzi...................................................7

2.1.5: Uboreshwaji wa Miundombinu ya Kiuchumi .......................................8

2.1.6: Ubinafsishaji ........................................................................................8

2.1.7: Uimarishaji wa Masoko na Ubia.........................................................9

2.1.8: Ushirika ...............................................................................................10

2.1.9: Matumizi Bora ya Ardhi......................................................................10

2.2 Madhumini ya Mkakati wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi..11

**SURA YA TATU ......................................................................... 12**

3.0 URATIBU WA UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA TAIFA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI...............................................................................12

3.1 Mfumo wa Uratibu wa Mkakati.............................................................12

3.2 Uratibu na Mgawanyo wa Majukumu....................................................13

3.2.1 Mkutano wa mwaka wa utambuzi wa wanaowezesha Wananchi Kiuchumi ....14
3.2.2 Kamati ya Taifa ya Ushauri wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ....14
3.2.3. Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ....17
3.2.4. Kamati za Uwezeshaji za Kisekta ....17
3.2. 5. Ofisi ya Rais- Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ....18
3.2. 6. Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa ....20
3.2.7. Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) ....21
3.2.8. Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ....23
3.2.9. Kamati ya Uwezeshaji ya Halmashauri ....23
3.2.10. Kamati ya Maendeleo ya Kata (WDC) ....26
3.2.11. Mkutano Mkuu wa Kijiji/Mtaa ....27
3.2.12. Kamati ya Uwezeshaji ya Kijiji/Mtaa ....28
3.2.13. Ngazi ya Familia ....29
3.3. Madawati ya Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania ....30
3.3.1 Dawati la Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania la Wizara ....30
3.3.2. Dawati la Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania la Mkoa ....31
3.3.3. Dawati la Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania la Halmashauri ....32
3.3.4. Dawati la Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania la Kata ....33
3.3.5. Dawati la Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania Ngazi ya ....35
Kijiji/Mtaa ....36

**SURA YA NNE .... 36**

4.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KATIKA UTEKELEZAJI WA MWONGOZO ....36

**SURA YA TANO .... 37**

5.0 UFUATILIAJI NA TATHMINI YA UWEZESHAJI ....37


# KAULI YA WAZIRI MKUU WA JAMHURI WA MUUNGANO WA TANZANIA



Serikali ikishirikiana na wadau mbalimbali kutoka Sekta Binafsi imekuwa ikitekeleza majukumu mbalimbali ya kuwawezesha Wananchi Kiuchumi. Ili uwezeshaji wa wananchi kufanyika kwa ufanisi na kumuwezesha mtanzania kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi na kumiliki rasilimali, kila kiongozi hana budi kuhakikisha kuwa rasilimali za Serikali na uwekezaji unaofanyika unalenga katika kuleta tija kwa nchi na wananchi kwa ujumla. Hii itawezekana tu pale ambapo viongozi watafuatilia miradi na uwekezaji unaofanyika katika maeneo yao ya kiutendaji ili kupata taarifa ambazo zitaisaidia Serikali kupima kama miradi na uwekezaji huo ina tija kwa jamii inayowazunguka na Taifa kwa ujumla.

Kumekuwa na changamoto kubwa ya kupata taarifa za utekelezaji hasa kuhusu jitihada mbalimbali zinazofanywa katika kuwawezesha wananchi kijamii na kiuchumi. Mwongozo huu wa Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Uwezeshaii Wananchi Kiuchumi ni nguzo kubwa ya maelekezo kwa Wizara, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Idara na Taasisi za Serikali na Sekta Binafsi kuweza kuwasilisha taarifa zao kwa Madawati ya Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania. Viongozi wahakikishe kuwa taarifa za utekelezaji wa miradi na uwekezaji katika maeneo yao zinalifikia Baraza la Taifa la Uwezesha Wananchi Kiuchumi kwa utaratibu ulioanishwa katika Mwongozo huu. Sote tufahamu kuwa taarifa hizi zitatoa picha ya mafanikio ya juhudi za Serikali katika kuwezesha wananchi wake kijamii na kiuchumi na kuzifanyia kazi changamoto zinazojitokeza ili kuleta ufanisi zaidi katika kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Ni matumaini yangu kuwa Watendaji wote wa kila Wizara, Idara za Serikali, Tawala za Mikoa na Serikali na Mitaa watakuwa wanatumia Mkakati wa Taifa wa Uwezeshaji na Mwongozo wake kama kiongozi muhimu wa kutekeleza masuala yote ya Uwezeshaji na Ushiriki wa Wananchi katika Uchumi wao. Aidha, Mwonzozo huu utaendelea kuimarisha utendaji na utekelezaji wa majukumu yote ya Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi kama yalivyoelekezwa katika Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 ambayo imetafsiriwa kiutendaji na Mkakati wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambao Mwongozo huu unatoa dira ya utekelezaji wake.



**MH. KASSIM MAJALIWA MAJALIWA (MB),**
WAZIRI MKUU,
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.

# DIBAJI




Mfumo wa kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 kupitia Mkakati wa Taifa wa Uwezeshaji Wanachi Kiuchumi ambao umeelezwa katika Mwongozo huu ni moja ya juhudi za Serikali katika kuhakikisha kuwa mipango ya Serikali inalenga katika kumuwezesha mwananchi kiuchumi ili kukuza uchumi na kuleta maendeleo kwa wananchi na Taifa kwa ujumla.

Mwongozo huu umeainisha majukumu ya kiutendaji katika kutekeleza Sera ya Taifa ya Uwezeshaji kuanzia ngazi ya kitaifa mpaka familia. Aidha, Mwonzozo umeelezea Mkakati wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambao umejikita katika nguzo tisa za Sera ya Taifa ya Uwezeshaji, mfumo wa uratibu, Kamati za Uratibu na Madawati ya Uwezeshaji na Ushiriki wa Wananchi ambayo yataanzishwa katika kila Wizara, Mikoa, Halmashauri, Kata na Vijiji/Mitaa.

Madhumuni ya Mwongozo huu yatafanikiwa iwapo wadau wote watashirikiana kwa pamoja katika kutekeleza kwa ufanisi shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi, kuibua na kuweka mikakati madhubuti katika kushughulikia changamoto za kiuwezeshaji katika maeneo yao, na hivyo kukidhi matarajio ya wananchi kuhusu uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Utekezaji wa Mwongozo huu unatumia mifumo ya kiutendaji iliyopo na haukusudii kuanzisha mfumo mpya kuanzia ngazi ya kitaifa hadi kijiji/mtaa. Ni matumaini yetu kuwa Viongozi wa Umma, Watumishi wa Umma, Sekta Binafsi, Wanataaluma, Asasi za Kiraia, Wananchi, Vyombo vya Habari na Wadau wengine watazingatia malengo, misingi ya utekelezaji na mambo mengine muhimu ya kuzingatia katika utekelezaji wa majukumu yao ya uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Ninawatakia utekelezaji mwema na wenye ufanisi.



**BIBI BENG'I M. ISSA,**
KATIBU MTENDAJI,
BARAZA LA TAIFA LA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI.

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Jitihada za kuhakikisha kuwa Uchumi wa Tanzania unamilikiwa na Wananchi zilianza mara baada ya kupata Uhuru (1961). Kabla na mara baada ya Uhuru sehemu kubwa ya uchumi wa nchi ilimilikiwa na Wageni/Wawekezaji. Mikakati mbalimbali iliandaliwa na kutekelezwa baada ya Uhuru ikiwa na lengo la kuhakikisha kuwa sehemu kubwa ya uchumi wa nchi inamilikiwa na Watanzania. Baadhi ya hatua zilizochukuliwa na Serikali ni pamoja na kuanzishwa kwa Azimio la Arusha (1967), Madaraka Mikoani (1972), Uanzishaji wa Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC), na Uanzishwaji wa Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo (SIDO 1973). Pamoja na hatua hizo mikakati zaidi iliendelea kuandaliwa kabla ya Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kutungwa mwaka 2004. Baadhi ya Mikakati hiyo ni pamoja na kuimarisha vyama vya Ushirika, uanzishwaji wa Sera ya Maendeleo ya Biashara Ndogo na za Kati (SMEs Development Policy-2003) na Sera ya Taasisi Ndogo Ndogo za Kifedha (National Micro-Finance Policy-2000). Hizi zote ni sera mtambuka ambazo utekelezaji wake unagusa sekta zote za uchumi na kijamii.

Ili kuweka msisitizo zaidi katika kuwawezesha wananchi kiuchumi, Serikali ilitunga Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004. Madhumuni ya Sera hii ni kutoa mwongozo wa kuhakikisha kwamba wananchi wanapata fursa za kiuchumi katika sekta mbalimbali. Kwa maana hiyo, Sera za Kisekta zitalenga katika kuwainua wananchi kwa kuwapa upendeleo wa makusudi ikibidi, na kuwawezesha kuwa na kauli na ushiriki kwenye shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) lilianzishwa mwaka 2005 kwa Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (Sheria na. 16 ya Mwaka 2004) chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Baraza hili ni chombo cha juu kitaifa cha kuratibu, kusimamia, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004. Ili kutekeleza majukumu yake kikamilifu Baraza limepewa mamlaka ya kuandaa Mikakati na Miongozo ya Uwezeshaji ya kitaifa inayohusisha sekta mbalimbali katika ngazi zote za kiutawala/kisera. Moja ya Mikakati hiyo ni Mkakati wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (National Multisectoral Strategic Framework

for Economic Empowerment). Mwongozai huu umeandaliwa ili kutoa maelekezo ya namna ya kutekeleza Mkakati huo.

Huu ni Mwongozo wa kitaifa kwa ajili ya kuwezesha uratibu, usimamizi, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Sera katika ngazi na sekta zote za kiuchumi kupitia Mkakati wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

### 1.1 Madhumuni ya mwongozo

Mwongozo huu una madhumuni yafuatayo:-

i. Kutoa maelekezo ya namna ya kutekeleza majukumu yaliyoainishwa katika Mkakati wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kuanzia ngazi ya Wizara, Mikoa, Halmashauri, Kata mpaka Vijiji/Mitaa.

ii. Kuainisha mfumo wa Uratibu na mgawanyo wa majukumu ya uwezeshaji kuanzia ngazi ya Kitaifa mpaka ngazi ya Familia;

iii. Kuainisha majukumu ya kamati mbalimbali za utekelezaji kuanzia ngazi ya Taifa hadi Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;

iv. Kuainisha majukumu ya Madawati ya Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania kuanzia ngazi ya Wizara, Mkoa, Halmashauri, Kata na Kijiji/Mtaa

v. Kufanikisha utekelezaji wa dhamira ya Serikali ya kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kuainisha majukumu ya uratibu katika kusimamia kwa karibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wanachi Kiuchumi kuanzia ngazi ya Taifa mpaka Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

### 1.2 Misingi ya Utekelezaji wa Mwongozo

Misingi ya utekelezaji wa Mwongozo huu uzingatie yafuatayo:

i. Kuwahudumia wananchi kwa ufanisi bila upendeleo pale wanapohitaji kuwezeshwa kupitia huduma tunazotoa katika utendaji wa kila siku;

ii. Kuratibu majukumu ya Uwezeshaji kwa kuzingatia uwajibikaji, uadilifu, uaminifu na kujali;

iii. Kila kiongozi atekeleze majukumu yaliyoainishwa katika ngazi yake ya kimamlaka na utekelezaji;

iv. Kila Kamati iliyoainishwa katika mwongozo ihakikishe inatekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa;

v. Kila Dawati la Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania lihakikishe kuwa linatekeleza majukumu yake hasa katika kufuatilia masuala ya Uwezeshaji, kuandaa taarifa na kuziwasilisha katika kamati husika kwa maafikiano na kuziwasilisha katika ngazi husika ili ziweze kulifikia Baraza la Taifa la Uwezeshaji;

vi. Kila kiongozi ahakikishe kuwa rasilimali zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya kiuwezeshaji zinaelekezwa katika miradi hiyo na kutumika kwa kuzingatia thamani ya pesa na vipaumbele vya miradi yenyewe;

vii. Kuepuka migongano ya kimaslahi katika kutekeleza masuala ya Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania katika mipango na miradi yote ya Uwezeshaji wananchi Kiuchumi;

viii. Kuhakikisha kuwa wananchi wanapewa upendeleo wa pekee na watoa huduma mbalimbali katika zabuni na miradi mikubwa katika maeneo yao pale wanapokidhi vijezo na masharti ya zabuni husika.

ix. Kufanya maamuzi kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu.

# SURA YA PILI

## 2.0 MKAKATI WA TAIFA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI.

Mkakati huu umeandaliwa kwa kushirikisha wadau mbalimbali kwa lengo la kufanikisha umiliki, uratibu, usimamizi, ufuatiliaji na tathmini ya Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Aidha, Mkakati umeainisha watendaji wakuu katika kila nguzo, majukumu yao, muda wa utekelezaji, matokeo ya kisekta na ya kitaifa.

Mkakati umezingatia nguzo kuu tisa (9) za Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kama ambavyo zimeelezwa hapa chini. Aidha, kila nguzo imebainisha watekelezaji wake, muda wa utekelezaji, matokeo (expected results) na viashiria (indicators) vya matokeo tarajiwa. Hata hivyo yapo maeneo ambayo kwa bahati mbaya baadhi ya taasisi tekelezi hazikuonekana kwenye orodha na nyingine pengine hazikuwepo wakati Mkakati unaandaliwa. Kutoonekana kwa taasisi hizo katika orodha ya watekelezaji hakuondoi haki na wajibu wao wa kutekeleza shughuli hizo za uwezeshaji. Matarajio yetu ni kuwa Mkakati utaendelea kurekebishwa na kuboreshwa kila mara kwa kushirikiana na wadau.

### 2.1 Nguzo za Mkakati wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

#### 2.1.1: Kukuza Uchumi na Kujenga Mazingira ya Uwekezaji

***Hoja:***

Kiwango cha ukuaji wa uchumi wa Tanzania ni kidogo na mazingira ya uwekezaji ambayo ndiyo chachu ya ukuaji wa uchumi endelevu ni hafifu.

***Tamko la Sera***

Jitihada za kuwawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za uchumi nchini ni muhimu ziendane na ukuaji wa uchumi unaojumuisha na kunufaisha Watanzania wengi, kuongeza vipato vyao pamoja na kuinua hali zao za kimaisha.

Kwa hoja na tamko la Sera ukuaji endelevu wa uchumi hauwezi kuwepo kama mazingira ya uwekezaji sio mazuri. Tangu mwaka 1985, wakati serikali ilipoamua kuingia kwenye uchumi huria, imelenga kuweka mikakati inayowezesha uwekezaji ndani ya nchi. Mikakati madhubuti ya kuboresha

mazingira ya uwekezaji inahitaji kuandaliwa na kutekelezwa na wadau wakuu katika nguzo hii ikiratibiwa na kusimamiwa na Wizara ya Fedha pamoja na taasisi nyingine zinazohusika.

***Washiriki wakuu*** katika jukumu hili ni pamoja na:

Wizara ya Fedha na Mipango; Benki Kuu ya Tanzania; Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; Wizara ya Katiba na Sheria; Wizara ya Kazi na Ajira; Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi; Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Wizara ya Maji na Umwagiliaji; Ofisi ya Rais -Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Taasisi za Dini; pamoja na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

### 2.1.2: Uboreshaji wa Mfumo wa Utozaji Kodi, Sheria, Kanuni, Leseni na Huduma Nyingine za Serikali

***Hoja***

- Pamoja na juhudi zinazoendelea za kuboresha mfumo wa kodi, bado mfumo na utawala wa kodi uliopo hautoi fursa inayowezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika uchumi.
- Baadhi ya sheria, kanuni na taratibu zilizopo haziendani na dhana ya uchumi wa Uwezeshaji.
- Upo udhaifu katika utoaji wa huduma mbalimbali zitolewazo na Serikali kwa wananchi.

***Tamko la Sera***

- Kuboresha mfumo na utawala wa kodi ili kuhamasisha uwekezaji.
- Kurekebisha sheria, kanuni na taratibu zilizopitwa na wakati ili ziendane na Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.
- Serikali itaboresha utoaji wa huduma kwa umma hasa katika kuwezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi. Aidha, watumishi watawezeshwa kuwa na mtazamo na fikra sahihi katika kutoa huduma za hali ya juu zitakazowezesha kusimamia vema uchumi katika mazingira ya utandawazi.

Mfumo mzuri wa Sheria na huduma bora kwa watumishi wa umma ni chachu kubwa ya kukuza uchumi kwa sababu unaweka mazingira bora ya uwekezaji

kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Vilevile Uboreshaji wa mfumo wa kodi na miundombinu utapanua wigo wa vyanzo vya mapato ya Taifa kwa ujumla na kuboresha huduma kwa jamii.

***Washiriki wakuu*** katika jukumu hili ni pamoja na:

Wizara ya Fedha na Mipango; Mamlaka ya Kodi Tanzania; Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Kituo cha Uwekezaji; Wizara ya Kazi na Ajira; Wizara ya Katiba na Sheria; Ofisi ya Waziri Mkuu; Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; pamoja na Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

### 2.1.3: Kukuza Mitaji

***Hoja***

Upatikanaji wa mitaji kwa wananchi ni mgumu kwa sababu ya:

(a) Ufinyu wa vyanzo vya akiba kutokana na kipato kidogo na kutokuwa na utamaduni wa kujiwekea akiba,

(b) Kuwepo kwa vizuizi vinavyosababisha mabenki kusita kutoa mikopo, mfano: gharama kubwa za kuhudumia utoaji mikopo (loan service charges) na kutokuwepo utaratibu wa kupata taarifa za mkopaji (Credit Reference Bureau), na

(c) Ukosefu wa ujuzi wa kuandaa maandiko ya biashara, ukosefu wa dhamana na mitaji ya kuanzisha miradi (taasisi nyingi za fedha zinakopesha miradi inayoendelea na si inayoanza)

***Tamko la sera***

Serikali itaweka mazingira mazuri ya upatikanaji wa mitaji kwa kuimarisha na kuboresha vyanzo vya akiba, itachukua hatua ya kuondoa vikwazo mbalimbali ili kuwezesha mabenki kukopesha kikamilifu amana zilizopo na kwa gharama nafuu, na itaweka mikakati ambayo utekelezaji wake utainua hali na hadhi ya wananchi ili wakopesheke.

Ili kuondokana na tatizo la ukosefu wa mitaji, Sera inahimiza ushirikiano wa wadau mbalimbali zikiwemo taasisi ndogondogo za fedha ili kubuni mbinu za kujiongezea mitaji; kuimarisha miundombinu itakayochochea maendeleo ya wawekezaji na kuweka mkakati wa kupunguza vikwazo vya kupata mitaji kutoka katika mabenki.

***Washiriki wakuu*** katika jukumu hili ni pamoja na:

Wizara ya Fedha na Mipango, Benki Kuu ya Tanzania; Mfuko wa Dhamana ya Uwekezaji Tanzania (UTT); Mifuko ya Pensheni; Mfuko wa Kudhamini Mikopo Tanzania; Benki ya Rasilimali; Mifuko ya Uwezeshaji; Benki za Biashara; Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; "Tanzania Association of Micro-finance Institutions" (TAMFI); na Ofisi ya Waziri Mkuu.

### 2.1.4: Kuinua Viwango vya Elimu Na Ujuzi

***<u>Hoja</u>***

Wananchi wanashindwa kushiriki katika shughuli za kiuchumi kwa vile wanakabiliwa na vikwazo vinavyotokana na elimu, ujuzi na uwezo mdogo kitaaluma. Kiwango kidogo cha elimu kinachangia baadhi ya wananchi kuendeleza mila na desturi potofu zisizo na upeo wa maendeleo. Aidha, mfumo wa elimu haujengi fursa ya uendelezaji wa ujasiriamali.

***<u>Tamko la Sera</u>***

Serikali itaangalia upya mfumo wa elimu kwa nia ya kuongeza kina cha mtazamo wa kisayansi ili kukabili mila na desturi potofu zinazodumaza maendeleao, na kumjenga Mwananchi anayejiamini, mbunifu na mwenye ari ya kuzalisha na kufanya biashara ama shughuli nyingine kwa umakini na ustadi mkubwa.

Mkakati huu unahimiza kuangalia upya mfumo mzima wa elimu, hususan, katika masuala ya sayansi na teknolojia ili kuwajengea wananchi uwezo wa kujiamini, kuwa wabunifu na **kuwa tayari kuwa wajasiriamali** na kujiajiri wenyewe pamoja na kutengeneza ajira kwa ajili ya wengine.

***Washiriki wakuu*** katika jukumu hili ni pamoja na:

Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi; Taasisi ya Elimu Tanzania (TIE); Tanzania Commission for Universities (TCU); Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA); Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; Shirika la Viwanda Vidogo (SIDO); Wizara ya Kazi na Ajira; Vyuo Vikuu; Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDC) pamoja na Mamlaka ya Elimu ya Ufundi Tanzania (VETA).

### 2.1.5: Uboreshwaji wa Miundombinu ya Kiuchumi

***Hoja***

Miundombinu ya kiuchumi hususan barabara, nishati, maji na mitandao ya mawasiliano ni nyenzo muhimu kwa maendeleo ya nchi. Uboreshaji wa eneo hili utapunguza umaskini kwa wananchi kwani utazalisha ajira; utaiwezesha nchi kuongeza wigo wake wa kufanya biashara za ndani na nje; utapunguza gharama za uzalishaji na bei za bidhaa zinazozalishwa na kuongeza upatikanaji wa huduma za afya na elimu; pamoja na kuhamasisha uwekezaji wa ndani na nje ya nchi.

***Tamko la Sera***

Serikali itatenga fedha na kushirikisha wadau wa maendeleo ili kuboreha miundombinu. Aidha, itaweka mazingira mazuri ya kuhamasisha sekta binafsi katika kuwekeza na kuendeleza miundombinu.

Ili kufanikisha hayo, taasisi mbalimbali hazina budi kushirikiana zikiongozwa na washiriki wakuu katika jukumu hili ambao ni;

Wizara ya Nishati na Madini; TANROADS; Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano; Shirika la Nyumba la Taifa (NHC); Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC); Kampuni ya Reli (TRL); Mamlaka ya Bandari; Mamlaka za Tawala za Mikoa; Bodi ya Mikopo; Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji; Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA); Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO); Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; Wizara ya Uchukuzi; Wizara ya Mawasiliano Sayansi na Teknolojia; Mamlaka ya Nishati Vijijini (REA); Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika; Wizara ya Maji; Mifuko ya Pensheni; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege.

### 2.1.6: Ubinafsishaji

***Hoja***

Njia mojawapo ya kuwapa wananchi fursa ya kushiriki na kumiliki mashirika ya umma na binafsi hususan yale yaliyobinafsishwa ni kununua hisa katika makampuni hayo.

***Tamko la Sera***

Serikali haina budi kuweka mkakati na mbinu zitakazowezesha wananchi kuelewa na kushawishika kununua hisa katika makampuni yaliyobinafsishwa na yale binafsi yaliyowekeza Tanzania kwa ajili ya kuimarisha uchumi wao. Ufanisi wa shughuli hiyo unatakiwa uandaaji wa mikakati, miongozo na taratibu ambazo taasisi zifuatazo zitahusika:

Wizara ya Fedha na Mipango, Benki Kuu Tanzania; Taasisi ya sekta Binafsi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Muungano wa Sekta Binafsi; Benki ya Rasilimali; Mifuko ya Pensheni; Mfuko wa Dhamana ya Uwekezaji Tanzania (UTT); Kituo cha Uwekezaji (TIC); Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE); Mamlaka ya Soko la Mitaji na Dhamana – "*Capital Markets and Securities Authority*".

### 2.1.7: Uimarishaji wa Masoko na Ubia

***Hoja***

Masoko yote ya ndani na nje sasa yanakabiliwa na ushindani mkali kutokana na utandawazi. Mara nyingi bidhaa zinazozalishwa nchini zinashindwa kupata masoko ya ndani na nje kwa sababu nyingi ikiwa ni pamoja na uwezo mdogo wa uzalishaji wa bidhaa za kutosha; kiwango cha chini cha ubora wa bidhaa zinazozalishwa nchini ambacho hakifikii viwango vya kimataifa; gharama kubwa ya uzalishaji mazao na bidhaa; vifungashio duni; ukosefu wa taarifa za masoko; kutokuendeleza masoko ya ndani; na kutotafuta masoko mapya nje ya yale yaliyozoeleka.

***Tamko la Sera***

Serikali itahakikisha kwamba taarifa kuhusu mwenendo wa masoko zinapatikana kwa wazalishaji na jitihada zaidi zinaendelezwa kuyafikia masoko ya ndani, nchi jirani na ya Soko la Dunia. Aidha, wananchi wanahimizwa kuzalisha mazao na bidhaa kulingana na matakwa ya soko.

Ili kutekeleza tamko hili, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ikishirikiana na taasisi zifuatazo itaandaa utaratibu wa kuhakikisha kuwa wigo wa masoko unapanuka. Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa; Bodi ya Leseni za Ghala; Kituo cha Uwekezaji Tanzania; TANTRADE; Bodi za Manunuzi za Wizara,

Taasisi za Serikali na mikoa; Shirika la Viwanda Vidogo vidogo; Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; pamoja na Export Processing Zones Authority (EPZA).

### 2.1.8: Ushirika

***Hoja***

Ushirika ni chimbuko la kujenga nguvu ya wananchi kuwa na sauti ya pamoja katika kufanya shughuli zao. Aidha, ushirika ni chombo madhubuti cha kuwawezesha wananchi hususan, wakulima, wafugaji, wafanyabiashara, wachimbaji madini, wavuvi na makundi mengine ambayo bila kuwepo katika ushirika itakuwa vigumu kwa mtu binafsi kuingia katika soko la ushindani au kuinua kipato chake. Licha ya kuwepo kwa jitihada za kuimarisha maendeleo ya Ushirika, bado kuna mapungufu yanayosababishwa na muundo mzima wa ushirika ikiwemo, elimu duni ya wanaushirika; ukosefu wa mitaji; kutoelewa dhana ya umiliki wa ushirika miongoni mwa wanaushirika; mtandao mdogo na kutokuweza kushindana katika soko.

***Tamko la Sera***

Serikali itaendelea kuimarisha ushirika nchini na kuhamasisha uundaji wa Ushirika mpya. Ili kushughulikia hoja na kutekeleza tamko la Sera kwa ukamilifu, taasisi zifuatazo ni vema zifanye kazi kwa pamoja ili kuandaa mikakati na miongozo mbalimbali:

Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi; Tume ya Maendeleo ya Ushirika; Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji; Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania; Mrajisi wa Vyama vya Ushirika; Benki Kuu ya Tanzania; Halmashauri za Wilaya; COASCO; TANTRADE; Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, na Chuo Kikuu Cha Ushirika Moshi.

### 2.1.9: Matumizi Bora ya Ardhi

***Hoja***

Wananchi hawajaweza kutumia Ardhi kikamilifu katika kujiwezesha na kuweza kushiriki katika shughuli za kiuchumi.

***Tamko la Sera***

Serikali inadhamiria kutumia Ardhi na Maliasili kama nyenzo muhimu za kumwezesha mwananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi. Hii

ni pamoja na kuhimiza matumizi ya Ardhi kama dhamana ya mikopo baada ya kurasimishwa.

Utekelezaji wa mkakati huu unahitaji ushirikiano wa karibu baina ya taasisi zifuatazo;

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi; Halmashauri za Wilaya, Serikali za Vijiji; Wizara ya Maliasili na Utalii; Tume ya Taifa ya Matumizi Bora ya Ardhi; Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano; Wizara ya Elimu, Tekinolojia na Ufundi; Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; Baraza la Taifa la Mazingira; na MKURABITA.

## 2.2 Madhumini ya Mkakati wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Madhumuni ya Mkakati wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ni pamoja na;

- Kutoa mwongozo na majukumu ya kila sekta na taasisi kuhusiana na uwezeshaji kiuchumi;
- Kuainisha kazi mahususi za uwezeshaji kiuchumi zitakazofanywa na kila taasisi husika ;
- Kutoa utaratibu wa jinsi ya kutekeleza kazi hizo;
- Kutoa viashiria na matokeo ya utekelezaji; pamoja na
- Utaratibu wa kufanya ufuatiliaji na tathmini ya shughuli zote za uwezeshaji kiuchumi.

# SURA YA TATU

## 3.0 URATIBU WA UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA TAIFA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

Utekelezaji wa Mkakati utafanywa na Wizara na Taasisi zake; Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) ikihusisha mikoa na Halmashauri katika ngazi zote; Sekta Binafsi pamoja na Wadau wa Maendeleo.


Mikoa, Halmashauri, Miji na Manispaa watawajibika kupanga mipango na bajeti kwa ajili ya kutekeleza shughuli za Uwezeshaji. Hata hivyo mipango yote ya Uwezeshaji inayotakiwa kutekelezwa na taasisi husika itaendelea kufanyika kuendana na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano; MKUKUTA II; pamoja na Mipango ya Sekta ya kila mwaka. Kwa taasisi ambazo zimeshaandaa mipango yao bila kipengele cha Uwezeshaji, zinashauriwa kurejea upya mipango yao ili kuingiza kipengele cha Uwezeshaji hasa katika kuhakikisha kuwa Madawati ya Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania yanatekeleza majukumu yake ipasavyo.

Baraza litaendelea na majukumu ya kuratibu, kusimamia, kufuatilia na kutathmini majukumu ya wadau wote kama ilivyoainishwa katika Mkakati.

### 3.1 Mfumo wa Uratibu wa Mkakati

Uratibu wa utekelezaji umepangwa kwa kuwa na kamati kuanzia ngazi ya Taifa hadi kijiji/mtaa na kila kamati ikiwa na majukumu yake kwa mtiririko endelevu. Kuanzia ngazi ya mkoa na kushuka chini, mfumo wa uratibu wa shughuli za Serikali uliopo utaendelea kutumiwa kukiwa na maboresho kwa kuanzisha Madawati ya Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania yatakayofanya kazi kwa niaba ya kamati za uratibu. Aidha, mkutano wa wadau wa tarehe 7 Mei, 2015 wa kutoa maoni ya kuboresha Rasimu ya Mwongozo walishauri mfumo wa uratibu uongeze Ngazi ya Familia kwa kuwa ndicho kiini cha Uwezeshaji. Mchoro na. 1 ukurasa wa 14 unaonyesha mfumo huu.

## 3.2 Uratibu na Mgawanyo wa Majukumu




*Mchoro 1: Mfumo wa Uratibu*

### 3.2.1 Mkutano wa mwaka wa utambuzi wa wanaowezesha Wananchi Kiuchumi

Kutakuwa na mkutano wa mwaka wa utambuzi wa wanaowezesha Wananchi Kiuchumi utakaofanyika kila mwaka. Mheshimiwa Waziri Mkuu ndiye atakuwa Mwenyekiti wa mkutano huo.

#### 3.2.1.1. Lengo kuu la Mkutano

Kuwakutanisha pamoja wadau wote wa uwezeshaji kiuchumi nchini kutoka sekta ya umma na binafsi kujadiliana kwa pamoja maendeleo ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na kutoa mapendekezo ya maboresho. Hii itaenda sambamba na kujenga mtandao wa wadau wanaotekeleza majukumu mbali mbali ya Uwezeshaji, uwasilishaji wa taarifa za utekelezaji wa majukumu hayo na maonesho ya shughuli mbalimbali za uwezeshaji.

#### 3.2.1.2. Majukumu ya Mkutano wa mwaka wa utambuzi wa wanaowezesha Wananchi Kiuchumi ni kama yafuatayo;

i. Kujadili taarifa ya utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kama itakavyowasilishwa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;

ii. Kutambua na kutunuku Wizara, Idara, Taasisi, Mikoa na Wilaya iliyofanya vizuri katika utekelezaji wa Sera ya Uwezeshaji kwa kuwapatia zawadi;

iii. Kuelekeza wadau mbalimbali katika kutekeleza changamoto zinazozuia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;

iv. Kuhamasisha juhudi mbali mbali za uwezeshaji wananchi kiuchumi,

**Washiriki wa Mkutano**: Wizara, Idara na Taasisi, Mikoa, Wilaya, Sekta Binafsi, Wabia wa Maendeleo, Mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, Watu binafsi.

**Wakati**: Mkutano huu unatarajiwa kufanyika kila mwaka.

### 3.2.2 Kamati ya Taifa ya Ushauri wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Kamati ya Taifa ya Ushauri wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi itahusisha wawakilishi toka sekta zote zinazotekeleza uwezeshaji kiuchumi zikiwemo

Wizara, Idara na Taasisi mbalimbali za umma na binafsi. Hiki ndicho chombo cha juu katika kutathmini na kushauri Mkakati kwa mtiririko maalum wa mipango, programu na miradi mbalimbali.

Kamati hii itapokea taarifa toka Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) litakalokusanya kwa niaba yake toka Kamati/Madawati za Uratibu za kisekta, na Madawati ya Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania ya mikoa na Halsmashauri.

#### 3.2.2.1 Majukumu ya Kamati ya Taifa ya Ushauri wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

i. Kutoa ushauri wa utekelezaji wa shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi kitaifa,
ii. Kuunganisha Wizara, Idara na Taasisi za umma na binafsi toka sekta zote za kiuchumi kwa ajili ya kuweka maazimio ya utekelezaji wa Mkakati wa Uwezeshaji,
iii. Kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa mkakati toka sekta zote husika na kutoa maelekezo/miongozo kwa sekta hizo,
iv. Kuishauri Serikali kuhusu hatua zaidi za kuboresha utekelezaji wa mkakati wa taifa wa uwezeshaji,

#### 3.2.2.2 Muundo wa Kamati ya Taifa ya Ushauri wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Wajumbe wa Kamati ya Kitaifa ya Uratibu itahusisha Wizara, Idara na Wakala za Serikali; Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Wataalam kutoka Sekta Binafsi; Mitandao ya Taasisi zisizo za Kiserikali na zile za Kijamii zinazojihusisha na masuala ya Kiuchumi; Wataalam kutoka taasisi za Elimu na Utafiti; Wawakilishi wa Wadau wa maendeleo. Kwa misingi hii, wajumbe watakuwa kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| KM OWM | Mwenyekiti |
| Katibu Mtendaji –NEEC | Katibu |
| Wataalam wa NEEC | Sekretarieti |

Wajumbe wengine ni Makatibu Wakuu wa Wizara zote zinazotekeleza Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi kiuchumi na taasisi nyingine kama ifuatavyo:

i. OR- TAMISEMI; Utumishi na Utawala Bora;
ii. Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira;
iii. OWM- Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Walemavu
iv. Wizara ya Fedha na Mipango;
v. Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi;
vi. Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano;
vii. Wizara ya Habari, Utamaduni, Wasanii na Michezo;
viii. Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi;
ix. Wizara ya Katiba na Sheria;
x. Wizara ya Nishati na Madini;
xi. Wizara ya Malia Asili na Utalii;
xii. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi;
xiii. Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji;
xiv. Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano Afrika Mashariki, Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa;
xv. Wizara ya Maji na Umwagiliaji;
xvi. Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto;
xvii. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa;
xviii. Wizara ya Mambo ya Ndani;
xix. Katibu Mkuu OR-TAMISEMI kwa nafasi ya pekee;
xx. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
xxi. Uwakilishi wa wadau wa maendeleo (Development Partners);
xxii. Sekta Binafsi (TPSF);
xxiii. Asasi za kiraia;
xxiv. Wanataaluma/ Taasisi za Tafiti;
xxv. Taasisi za kifedha (TBA/TAMFI);
xxvi. Asasi zisizo za Kiserikali (AZISE);
xxvii. Wawakilishi wa makundi yenye mahitaji maalum.

### 3.2.3. Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) lilianzishwa kwa Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (Sheria na. 16 ya Mwaka 2004) chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Baraza limeundwa na Sekretariaeti ambayo inafuatilia na kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004. Baraza limepewa mamlaka kisheria ya kusimamia, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mikakati na Miongozo ya Uwezeshaji katika sekta mbalimbali katika ngazi zote za kiutawala/kisera na sekta binafsi. Sekretarieti ina wajibika kwa Baraza ambacho ndicho chombo cha juu zaidi.

#### 3.2.3.1. Lengo la Baraza

Baraza limeundwa ili kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004. Baraza lina wajibu wa uratibu, usimamizi, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Sera katika ngazi na sekta zote za kiuchumi kupitia Mkakati wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

#### 3.2.3.2. Majukumu ya Baraza kwenye Mwongozo:-

i. Kufuatilia taarifa zote za utekelezaji wa shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi kitaifa;
ii. Kuchambua taarifa za utekelezaji wa shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi kutoka Wizara, Idara na Taasisi za umma, binafsi na sekta zote za kiuchumi kwa ajili ya kuweka maazimio ya utekelezaji wa Mkakati wa Uwezeshaji;
iii. Kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa mkakati toka sekta zote husika na kutoa maelekezo/miongozo kwa sekta hizo;
iv. Kufuatilia uondoaji wa changamoto zinazofanya wananchi wasisishiriki kwenye fursa za kiuchumi; na
v. Kuandaa agenda za mkutano wa kitaifa wa mwaka wa utambuzi wa wanaowezesha Wananchi Kiuchumi.

### 3.2.4. Kamati za Uwezeshaji za Kisekta

Ngazi hii inahusisha sekta zote kwa kuzingatia nguzo tisa (9) za Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi zikihusisha pia Wizara zinazohusika katika utekelezaji.

### 3.2.4.1. Muundo wa Kamati za Uwezeshaji za Kisekta

Katika Wizara, Katibu Mkuu atakuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Uwezeshaji na atateua wajumbe wa kamati wapatao watano (5) na kati yao apatikane mmoja atakayeratibu majukumu katika Dawati la Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania Wizarani hapo.

### 3.2.4.2. Majukumu ya Kamati za Kisekta

i. Kuhakikisha kuwa Sera, Sheria, Miongozo na Mikakati ya sekta husika inahuisha suala la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;

ii. Kuratibu utekelezaji wa Mkakati katika Wizara yake (taasisi zilizo chini yake, masuala ya sekta yake katika Serikali za Mitaa);

iii. Kuhakikisha kuwa Wizara yake inaweka majukumu ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ili kuibua fursa kwa watanzania katika mipango na kuitekeleza ipasavyo;

iv. Kuhakikisha kuwa shughuli za uwezeshaji za Wizara yake kwa mujibu wa Mkakati zinatengewa bajeti na inatumika kwa usahihi;

v. Kuhakikisha kuwa Wizara yake inatoa kipaumbele (preferential treatment) kwa watanzania katika utoaji wa zabuni zake;

vi. Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa shughuli za uwezeshaji za sekta husika katika mikoa na wilaya na kuwasilisha taarifa zake kwa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;

vii. Kutafsiri taarifa za utekelezaji za kisekta katika kumwezesha na kumshirikisha Mtanzania kiuchumi;

viii. Kushiriki kikamilifu katika mkutano wa Kitaifa wa utambuzi wa wanaowezesha Wananchi Kiuchumi; na

ix. Kushirikiana na TAMISEMI kuhakikisha kuwa utekelezaji wa Sera za sekta husika zinawafikia walengwa katika ngazi ya Kijiji na familia.

### 3.2. 5. Ofisi ya Rais- Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

Ofisi ya Rais - TAMISEMI ndiyo yenye dhamana kwa mikoa na serikali za mitaa. Ikishirikiana na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi watafanya kazi na Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC), Kamati ya Uwezeshaji

ya Halmashauri, Kamati ya Maendeleo ya Kata (WDC) na Kijiji/Mtaa katika kuhakikisha utekelezaji wa Mkakati.

#### 3.2.5.1. Majukumu ya OR-TAMISEMI

Katika kuratibu utekelezaji, OR-TAMISEMI itahakikisha kuwa;

i. Madawati ya Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania yanaanzishwa katika kila Mkoa na Halmashauri;

ii. Kila Dawati la Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania la mkoa linashirikiana vema na Kamati ya Ushauri ya kila Mkoa na Halmashauri katika utekelezaji wa Mkakati;

iii. Kila Dawati la Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania la Halmashauri linashirikiana vema na Kamati ya Uwezeshaji ya Halmashauri katika kutekeleza Mkakati;

iv. Kila mkoa na Halmashauri wanatenga bajeti za utekelezaji wa masuala ya uwezeshaji kiuchumi kama yalivyoainishwa katika Mkakati;

v. Zabuni mbalimbali za OR-TAMISEMI, Mikoa na Halmashauri zinatoa kipaumbele kwa Watanzania wenye sifa na uwezo;

vi. Kila Halmashauri inatenga asilimia kumi ya mapato yake yote kwa ajili ya mfuko wa uwezeshaji wa wanawake (5%) na wa vijana (5%);

vii. Mikoa na Halmashauri wanatenga maeneo maalum ya uwezeshaji kwa ajili ya shughuli za uwezeshaji kiuchumi zikiwemo kilimo, viwanda na biashara ndogo na za kati;

viii. Halmashauri husika zinaweka mipango ya matumizi bora ya ardhi katika maeneo yake na hivyo kupanga matumizi ya ardhi kwa shughuli za kiuchumi na kijamii ili kuepusha migogoro ya ardhi kati ya wananchi hususan Wakulima na Wafugaji;

ix. Mikoa na Halmashauri kuhakikisha maeneo yanayotengwa yana huduma za msingi/muhimu, mfano; Maji, Umeme, Miundombinu ya barabara na kuhifadhi;

x. Mikoa na Halmashauri kuhakikisha wanatengeneza mazingira rafiki ya kuwawezesha wananchi kiuchumi, (umuhimu wa kuwepo one stop centre);

xi. Utekelezaji wa Mkakati unafanyika katika mtiririko sahihi toka ngazi

ya kijiji hadi mkoa kama unavyoelekezwa na Mkakati;

xii. Utekelezaji wa Sheria, Sera, Kanuni zinazoelekeza kuhusu Uwezeshaji wananchi Kiuchumi unafanyika katika mikoa na wilaya zake;

xiii. Sheria ndogo ndogo katika ngazi ya Halmashauri zinahakikiwa (zinahuishwa) ili ziende sambamba na Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Dhana yake;

xiv. Wadau wote wanaofanya tafiti za masuala mbalimbali ya uwezeshaji wananchi kiuchumi wapewe kibali kutoka kwa Katibu Mkuu OR – TAMISEMI na kufuatilia matokeo ya tafiti hizo;

xv. OR-TAMISEMI/Mikoa wanashirikiana na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi katika kufuatilia Utekelezaji wa Shughuli za Uwezeshaji katika MSM (Mikoa na Serikali za Mitaa)

xvi. Kila Mkoa na Halmashauri wanahamasisha wananchi kujiunga katika vikundi vya Uwezeshaji kama VICOBA na SACCOS ili kujenga utashi wa kujiwekea akiba na kukopa kwa ajili ya mitaji ya kuendeleza shughuli za uwekezaji katika maeneo yao;

xvii. Utekelezaji wa masuala ya Uwezeshaji katika Mikoa na Halmashauri yanashirikisha sekta ya umma na binafsi;

xviii. Uwekezaji kwenye miradi mikubwa katika Mikoa na Halmashauri unatoa fursa kwa wazalendo kushiriki, hususan, katika miundombinu;

xix. Mikoa na Halmashauri ina orodha hai ya wadau wa Uwezeshaji (taasisi na miradi) na kuzifikisha kwa wananchi ili waweze kufaidika na huduma zake; na

xx. Mikoa na Halmashauri wanaandaa taarifa za Uwezeshaji na kuziwasilisha Baraza la Taifa la Uwezeshaji na TAMISEMI.

### 3.2. 6. Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa

Katibu Tawala wa Mkoa ndiye msimamizi mkuu wa utekelezaji wa masuala ya uwezeshaji wananchi kiuchumi katika mkoa wake.

#### 3.2.6.1. Majukumu ya Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa

i. Kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa masuala ya uwezeshaji wananchi kiuchumi katika mkoa wake;

ii. Kuteua na kumsimamia mratibu wa uwezeshaji wananchi kiuchumi

wa mkoa ambaye ni Katibu Tawala Msaidizi Sehemu ya Uchumi na Uzalishaji;

iii. Kuhakikisha kuwa Dawati la Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania la mkoa linafanya kazi zake bega kwa bega na kamati ya uwezeshaji ya mkoa;

### 3.2.7. Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC)

Kamati ya Ushauri ya Mkoa itawajibika kuratibu shughuli za uwezeshaji katika mkoa. Madawati ya Uwezeshaji katika kila mkoa yanatakiwa kuwepo na yatafanya uratibu wa shughuli za uwezeshaji katika mikoa yao kwa niaba ya Kamati ya Ushauri ya Mkoa ambayo itawasilisha taarifa zake za ujumla kwa Baraza la Taifa la Uwezeshaji na nakala kwa Katibu Mkuu OR-TAMISEMI. Kwa kuwa mikoa hutekeleza majukumu ya sekta mbalimbali, itaandaa pia taarifa za Uwezeshaji za kisekta na kuwasilisha kwa Wizara husika kutegemeana na sekta. Ngazi ya Mkoa itaratibu na kupata taarifa toka Halmashauri za wilaya zake. Katika Mikoa, Ofisi ya Katibu Tawala Msaidizi - Serikali za Mitaa ndiyo itaratibu Dawati la Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania la mkoa.

#### 3.2.7.1. Muundo wa Kamati ya Ushauri ya Mkoa

Kamati hii itajumuisha wajumbe wafuatao:

| | |
|---|---|
| Mwenyekiti | Mkuu wa Mkoa |
| Katibu: | Katibu Tawala wa Mkoa |

Wajumbe wengine ni Wakuu wa idara katika ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri, Wenyeviti wa Halmashauri, Wabunge wote wa majimbo katika mkoa, Wawakilishi wa dini, Wawakilishi wa vyama visivyo vya kiserikali na vya kijamii. Pia Afisa Mipango/Mchumi wa Halmashauri aambatane na Mkurugenzi wake.

#### 3.2.7.2. Majukumu ya Kamati ya Ushauri ya Mkoa

i. Kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi katika mkoa husika;

ii. Kuhakikisha uwepo wa Dawati la Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania la Mkoa na kuteua Mratibu wa Uwezeshaji Mkoa katika nafasi hiyo ambaye atafanya kazi kwa niaba ya Kamati;

iii. Kuhakikisha uwepo wa Madawati ya Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania ya Halmashauri na yanatekeleza majukumu yake chini ya Kamati za Uwezeshaji za Halmashauri zilizopo mkoani kama yalivyoainishwa katika mkakati;

iv. Kuhakikisha kuwa mkoa na Halmashauri zake zinaweka masuala ya uwezeshaji kiuchumi katika mipango (mpango mkakati, mpango kazi) yao kama ilivyoainishwa katika mkakati;

v. Kuhakikisha kuwa kazi za uwezeshaji kiuchumi (za mkoa na Halmashauri zake) zinatengewa bajeti kila mwaka;

vi. Kufuatilia na kuhakikisha kuwa bajeti za uwezeshaji za mkoa na Halmashauri zake zinatumika kama ilivyokusudiwa;

vii. Kuhakikisha kuwa Sera, Mkakati wa Taifa, Sheria na miongozo mingine ya uwezeshaji wananchi kiuchumi vinawafikia wadau na wananchi kwa ujumla;

viii. Kuhakikisha uwepo wa orodha hai ya wadau wa uwezeshaji kiuchumi katika mkoa na wananchi wanafaidika na huduma zao;

ix. Kuhakikisha kuwa, Halmashauri zinatenga fedha kwa ajili ya mipango ya matumizi bora ya ardhi katika maeneo yake na hivyo kupanga matumizi ya ardhi kwa shughuli za kiuchumi na kijamii ili kuepusha migogoro ya ardhi kati ya wananchi (hususan Wakulima na Wafugaji) na kutoa fursa kwa ajili ya makundi maalum kama vijana, wajasiriamali wadogo, wanawake na watu wenye ulemavu.

x. Maeneo yanayotengwa na Halmashauri yana huduma za msingi/ muhimu, mfano; Maji, Umeme, Miundombinu ya barabara na kuhifadhi;

xi. Halmashauri wanatengeneza mazingira rafiki ya kuwawezesha wananchi kiuchumi, (umuhimu wa kuwepo **'one stop centre'**).

xii. Kuhakikisha kuwa utekelezaji wa masuala ya Uwezeshaji katika Mkoa na Halmashauri yanashirikisha sekta ya umma na binafsi;

xiii. Kuhakikisha kuwa uwekezaji kwenye miradi mikubwa katika Mkoa na Halmashauri unatoa fursa kwa wazalendo kushiriki, hususan, katika miundombinu;

xiv. Kuhakikisha kuwa utoaji wa Zabuni mbalimbali za Mkoa na Halmashauri utatoa kipaumbele kwa watanzania wenye sifa;

xv. Kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Uwezeshaji za mkoa (ikujumuisha Halmashauri zake); na

xvi. Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa shughuli za uwezeshaji (ikizingatia shughuli za wadau wote wa uwezeshaji katika Halmashauri zote) katika mkoa na kuwasilisha taarifa kwa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kila mwezi Juni na Desemba,

### 3.2.8. Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri

Mkurugenzi wa halmashauri ndiye msimamizi mkuu wa utekelezajia wa masuala ya uwezeshaji wananchi kiuchumi katika Halmashauri yake.

### 3.2.8.1 Majukumu Mkurugenzi wa Halmashauri

i. Kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa masuala ya uwezeshaji wananchi kiuchumi katika Halmashauri yake;

ii. Kuteua na kumsimamia mratibu wa uwezeshaji wananchi kiuchumi wa Halmashauri ambaye ni afisa maendeleo ya jamii;

iii. Kuhakikisha kuwa Dawati la Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania la Halmashauri linafanya kazi zake bega kwa bega na kamati ya uwezeshaji ya Halmashauri;

iv. Kuwezesha Baraza la Mamlaka ya Mji Mdogo katika Halmashauri yake kujadili na kuhakikisha utekelezaji wa masuala ya uwezashaji wananchi kiuchumi katika eneo lao na kuwasilisha katika Vikao vya Baraza la Madiwani.

### 3.2.9. Kamati ya Uwezeshaji ya Halmashauri

Kamati ya kudumu ya Ujenzi, Uchumi na Mazingira katika Halmashauri itaratibu shughuli zote za uwezeshaji kiuchumi katika Halmashauri. Dawati la Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania la Halmashauri litafanya kazi kwa niaba ya Kamati hii na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji kwake. Kamati itahakikisha kuwa shughuli za uwezeshaji kiuchumi zinapewa rasilimali za kutosha kutoka katika bajeti ya Halmashauri.

#### 3.2.9.1. Muundo wa Kamati ya Uwezeshaji ya Halmashauri

Kamati hii huundwa na baadhi ya madiwani katika Halmashauri na kati yao huchaguliwa mwenyekiti na wengine kubaki wajumbe. Katibu wa kamati ni Mkurugenzi wa Halmashauri na huambatana na watendaji wake toka idara zinazohusika na kamati.

#### 3.2.9.2. Majukumu ya Kamati ya Uwezeshaji Ngazi ya Halmashauri (Kamati ya Ujenzi, Uchumi na Mazingira)

i. Kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi katika Halmashauri husika;

ii. Kuhakikisha uwepo wa Dawati la Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania katika Halmashauri ambalo litafanya kazi kwa niaba ya Kamati;

iii. Kuhakikisha kuwa Dawati la Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania la Halmashauri linatekeleza majukumu yake chini ya Kamati kama yalivyoainishwa katika Mwongozo na Mkakati;

iv. Kuhakikisha kuwa Halmashauri zinajumuisha mipango yote ya kata inayohusu Uwezeshaji katika mipango yake (mpango mkakati, mpango kazi) yao kama ilivyoainishwa kwenye Mkakati;

v. Kuhakikisha kuwa kazi za uwezeshaji kiuchumi (za Halmashauri na kata zake) zinatengewa bajeti kila mwaka;

vi. Kufuatilia na kuhakikisha kuwa bajeti za uwezeshaji za halmashauri na kata zake zinatumika kama ilivyokusudiwa;

vii. Kuhakikisha kuwa Sera, Mkakati wa Taifa, Sheria na miongozo mingine ya uwezeshaji wananchi kiuchumi inawafikia wadau na wananchi kwa ujumla;

viii. Kuhakikisha uwepo wa orodha hai ya wadau wa uwezeshaji kiuchumi katika Halmashauri na ziwafikie wananchi ili waweze kufaidika na huduma zao;

ix. Kuweka mkazo katika Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wananchi mijini na vijijni katika Halmashauri husika;

x. Kuhakikisha kuwa Halmashauri na kata zake zinatenga maeneo maalum ya maendeleo (kilimo, biashara, viwanda vidogo) kwa ajili ya vijana,

xi. Kuhakikisha kuwa Halmashauri inatenga asilimia kumi (10%) ya mapato yake yote kwa ajili ya mfuko wa maendeleo wa wanawake (5%) na wa vijana (5%) na kuhakikisha fedha hizo zinakopeshwa kwa walengwa baada ya kujiridhisha kuwa walengwa wana sifa za kukopeshwa kwa sababu mfuko huo ni endelevu (revolving fund) hivyo ni lazima kila anayekopesshwa arejeshe ili kutoa fursa kwa wengine.

xii. Kuhakikisha kuwa Halmashauri imetenga maeneo rasmi ya Ardhi kwa ajili ya wafugaji na Wakulima ili kuleta mahusiano mazuri kati ya makundi hayo;

xiii. Kuhakikisha kuwa Halmashauri inahusisha suala la hifadhi ya Mazingira na mabadiliko ya Tabia Nchi katika Mipango ya Maendeleo ya Wilaya ili kuboresha mazingira ambayo ni muhimu katika suala zima la uzalishaji wa mazao ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi;

xiv. Kuhakikisha kuwa utekelezaji wa masuala ya Uwezeshaji katika Halmashauri unashirikisha sekta ya umma na binafsi;

xv. Kuhakikisha kuwa uwekezaji kwenye miradi mikubwa katika Halmashauri unatoa fursa kwa wazalendo kushiriki, hususan, katika miundombinu;

xvi. Kuhakikisha kuwa utoaji wa Zabuni mbalimbali za Halmashauri utatoa kipaumbele kwa watanzania wenye sifa na uwezo;

xvii. Kuhakikisha kuwa Halmashauri ina orodha hai ya wadau (taasisi na miradi) ili wananchi waweze kufaidika na huduma zake;

xviii. Kuhakikisha upatikanaji wa masoko ya bidhaa za kiuchumi hususan masoko ya mazao ya kilimo na ufugaji;

xix. Kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Uwezeshaji za Halmashauri;

xx. Kujadili na kutoa mwelekeo wa namna bora ya kukabiliana na changamoto za kiuwekezaji ndani ya Halmashauri mfano;- migogoro ya wawekezaji na wakazi, utoaji wa vibali vya kutumia rasilimali za

vijiji/Halmashauri na leseni za biashara;

xxi. Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa shughuli za uwezeshaji (ikizingatia shughuli za wadau wote wa uwezeshaji katika Halmashauri na kata zote pamoja na sekta binafsi) na kuwasilisha taarifa katika kikao cha Baraza la Madiwani, Kamati ya Ushauri ya Wilaya(DCC) na hatimaye ngazi ya Mkoa

### 3.2.10. Kamati ya Maendeleo ya Kata (WDC)

Kamati ya Maendeleo ya Kata (WDC) itaratibu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi katika kata kwa kufuatilia vijiji/mitaa v/yote ndani ya kata husika. Taarifa ya utekelezaji itawasilishwa kwa **Kamati ya Uwezeshaji ya Halmashauri**.

### 3.2.10.1. Muundo wa Kamati ya Maendeleo ya Kata

| | |
|---|---|
| Mwenyekiti | Mh. Diwani wa kata, |
| Katibu | Afisa Mtendaji Kata, |

Wajumbe wengine ni Wenyeviti wa vijiji/mitaa, Afisa Watendaji wa vijiji/mitaa, Wataalam wa kata na wa vijiji/mitaa, Diwani wa viti maalumu mkazi wa kata husika. Pia Watu maarufu katika eneo husika ni wajumbe lakini hawatakuwa na uwezo/fursa ya kupiga kura.

### 3.2.10.2 Majukumu ya Kamati ya Maendeleo ya Kata

i. Kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi katika kata husika;

ii. Kuhakikisha uwepo wa mtaalam katika kata atakayeratibu utekelezaji wa majukumu ya uwezeshaji katika ngazi hii na kutoa taarifa kwa kamati;

iii. Kuhakikisha kuwa mratibu wa uwezeshaji kata na waratibu wa uwezeshaji wa vijiji/mitaa katika kata husika wanatekeleza majukumu yao kama yalivyoainishwa katika mkakati;

iv. Kuhakikisha kuwa kata na mitaa au vijiji vinaingiza masuala ya uwezeshaji kiuchumi katika mipango na bajeti zao kila mwaka;

v. Kufuatilia na kuhakikisha kuwa bajeti za uwezeshaji za kata na vijiji/mitaa yake zinatumika kama ilivyokusudiwa;

vi. Kuhakikisha kuwa Sera, Mkakati wa Taifa, Sheria na miongozo mingine ya uwezeshaji wananchi kiuchumi inawafikia wadau na wananchi kwa ujumla katika kata;

vii. Kuhakikisha uwepo wa orodha hai ya wadau wa uwezeshaji kiuchumi katika kata na wananchi wanafaidika na huduma zao;

viii. Kuhakikisha kuwa kata na vijiji/mitaa v/yake zinatenga maeneo maalum ya maendeleo (kilimo, biashara, viwanda vidogo) kwa ajili ya vijana;

ix. Kufuatilia na kutathimini utekelezaji wa shughuli za uwezeshaji katika vijiji/mitaa na kuwasilisha taarifa zao kwa Halmashauri kila robo mwaka.

### 3.2.11. Mkutano Mkuu wa Kijiji/Mtaa

Huu ndio mkutano unaofikia Mwananchi moja kwa moja katika vijiji/mitaa ambako ndiko ziliko shughuli za kiuchumi. Mkutano Mkuu wa Kijiji ndicho chombo cha juu kabisa cha utawala katika kijiji.

Katika ngazi hii Halmashauri ya kijiji ambayo hukutana kila mwezi itaratibu na kusimamia shughuli zote za uwezeshaji kiuchumi kijijini na kupeleka taarifa kwa Mkutano Mkuu wa kijiji ambao hufanyika kila robo mwaka.

#### 3.2.11.1. Muundo wa Mkutano Mkuu wa Kijiji/Mtaa

| | |
|---|---|
| **Mwenyekiti** | Mwenyekiti wa kijiji/mtaa, |
| **Katibu** | Afisa Mtendaji wa kijiji/mtaa, |
| **Wajumbe** | Wanakijiji wote wenye umri usiopungua miaka kumi na nane (18). |

#### 3.2.11.2. Majukumu ya Mkutano Mkuu wa Kijiji/Mtaa

i. Kupokea taarifa ya Uwezeshaji Kiuchumi ya kijiji au mtaa kutoka Kamati ya Uwezeshaji ya Kijiji/Mtaa;

ii. Kujadili taarifa ya Uwezeshaji Kiuchumi ya kijiji au Mtaa itakayoletwa na Kamati ya Uwezeshaji ya Kijiji/Mtaa;

iii. Kuhamasisha wana Kijiji au Mtaa kushiriki kikamilifu kwenye fursa za Uwezeshaji kiuchumi zilizopo katika eneo husika;

iv. Kuelezea utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi katika kijiji au mtaa husika; na

v. Kujadili changamoto zilizopo katika ushiriki wa familia katika Uwezeshaji wananchi kiuchumi na kuziwasilisha kwenye ngazi ya juu kwa hatua zinazofaa.

### 3.2.12. Kamati ya Uwezeshaji ya Kijiji/Mtaa

**Mwenyekiti** Mwenyekiti wa kijiji/mtaa,

**Katibu** Afisa Mtendaji wa kijiji/mtaa,

**Wajumbe Wengine wa Kamati ya Uwezeshaji katika Kijiji/Mtaa ni** Wenyeviti wa Vitongoji na wajumbe wengine wakiwemo wanawake wasiopungua theluthi moja ya wajumbe wote.

#### 3.2.12.1. Majukumu ya Kamati ya Uwezeshaji ya Kijiji/Mtaa

i. Itahakikisha uwepo wa mtaalam katika kijiji/mtaa atakayeratibu utekelezaji wa majukumu ya uwezeshaji katika ngazi hii;

ii. Itatoa ushirikiano kwa mratibu wa uwezeshaji katika kijiji/mtaa ili aweze kufanya kazi za uwezeshaji kiuchumi kwa ufanisi;

iii. Itahakikisha kuwa wanawake na vijana katika kijiji/mtaa wanashiriki katika shughuli za kiuchumi ipasavyo na kufikiwa na mifuko yao ya maendeleo ya kiuchumi iliyopo wilayani;

iv. Kutenga maeneo maalum kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi zikiwemo biashara ndogondogo za vijana na wanawake;

v. Kuhamasisha na kuwezesha maendeleo ya vikundi vya kiuchumi kama SACCOS na VICOBA katika kijiji/mtaa husika;

vi. Kuweka malengo ya uzalishaji mali kwa kila mwanachi aliyefikia umri wa miaka kumi na nane (18), na kuweka sheria ndogondogo za kuwabana wale wasiotaka kujishughulisha; na

vii. Kuhakikisha kuwa taarifa za Uwezeshaji za kijiji/mitaa zinawasilishwa katika Mkutano Mkuu wa Kijiji/Mtaa na baadaye katika ngazi ya Kata;

### 3.2.13. Ngazi ya Familia

Hawa ndio walengwa halisi wa uwezeshaji kiuchumi. Mfumo huu unalenga kuhakikisha kuwa kila mwananchi mwenye umri wa miaka kumi na nane (18) na kuendelea ajishughulishe kiuchumi. Kiongozi wa familia atawajibika kuhakikisha kuwa familia inajishughulisha kiuchumi na mchango wa kila mwanafamilia unaonekana. Kila Mwenyekiti wa Kijiji au Mtaa atatakiwa kuhamasisha wananchi wake kutekeleza majukumu yake kwa utashi wa kiuwezeshaji kwa kutumia fursa zinazowazunguka. Hii iwe ni kampeni maalum katika mikutano yote ya kijiji na ikiwezekana kuwe na uhamasishaji wa nyumba kwa nyumba.

Uwezeshaji katika familia utatofautiana kulingana na fursa zilizopo kwa kila familia. Pamoja na tofauti za fursa zilizopo kwa kila familia na majukumu mengine ya kiuwezeshaji, familia zijikite katika kutekeleza Mkakati wa Uwezeshaji kwa:

i. Kuanzisha/kuendeleza shughuli za kiuchumi kama vile biashara, kilimo, ufugaji, uongezaji thamani (usindikaji), sanaa za mikono, n.k,

ii. Kuhakikisha kuwa watoto wanaandikishwa shule katika umri unaokubalika kisheria na wanashiriki masomo ipasavyo;

iii. Watoto washirikishwe katika kufanya kazi za familia ili kuwajengea ari ya kufanya kazi na kujitegemea,

iv. Watoto wahimizwe na kuwezeshwa kuanzisha miradi midogomidogo ya kimaendeleo kama Kilimo cha bustani na ufugaji wa mifugo kama kuku, mbuzi, sungura, n.k,

v. Kuhimiza utashi na desturi ya kujiwekea akiba, wazazi wawahimize watoto kujiwekea akiba kwa njia ya VICOBA, SACCOS na kuwafungulia akaunti za watoto katika Mabenki,

vi. Kuhakikisha kuwa familia ina eneo la ardhi la kutosha, hasa kwa walio vijijini. Ardhi itawawezesha kufanya shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwemo Kilimo na ufugaji, na

vii. Kuwa na mikutano ya kifamilia kujadili maendeleo na changamoto za utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya kifamilia na kufundisha maadili kwa watoto.

### 3.3. Madawati ya Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania

Madawati ya Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania yataanzishwa katika ngazi zote za uratibu na utekelezaji katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Idara za Kisekta, Kamati ya Ushauri ya Mkoa na Kamati ya Uwezeshaji ya Halmashauri). Madawati haya yatakuwa na jukumu la kuratibu utekelezaji wa shughuli za Uwezeshaji kwa niaba ya kamati na kuwasilisha taarifa kwa kamati hizo. Dawati la Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania kwa kila Taasisi (Wizara, Idara, Wakala, TAMISEMI) litaratibiwa na Idara ya Maendeleo ya Jamii. Kwa zile taasisi ambazo hakuna Idara ya Maendeleo ya Jamii, Mkuu wa Taasisi atateua Idara ambayo itakuwa na Mtaalam Mwandamizi ambaye atakuwa anaratibu utekelezaji wa Shughuli za Uwezeshaji katika taasisi husika.

#### 3.3.1 Dawati la Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania la Wizara

Kutakuwa na Dawati la Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania katika kila Wizara inayotekeleza Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Dawati hili litakuwa na jukumu la kuratibu utekelezaji wa shughuli za Uwezeshaji katika Wizara zikiwemo zifanywazo na idara, taasisi na wakala zilizo chini ya Wizara husika kwa niaba ya Kamati ya Uwezeshaji ya Wizara na kuwasilisha taarifa kwa kamati hizo.

##### 3.3.1.1. Majukumu ya Dawati la Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania katika Wizara

Madawati ya Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania katika Wizara yatakuwa na shughuli zifuatazo:

i. Kuhakikisha utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kuratibu, kusimamia na kufuatilia shughuli za uwezeshaji zinazofanywa katika Wizara kwa niaba ya Kamati ya Uwezeshaji ya Wizara;

ii. Kuandaa bajeti kwa ajili ya kufuatilia utekelezaji wa Sera hiyo;

iii. Kufuatilia na kupokea taarifa za utekelezaji wa Sera toka kwa sekta husika;

iv. Kutafsiri mafanikio ya kisekta katika kumwezesha Mtanzania kiuchumi;

v. Kutoa ushauri kuhusu masuala ya uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa Kamati ya Uwezeshaji ya Wizara;

vi. Kupokea maelekezo toka kwa Kamati ya Uwezeshaji ya Wizara na kuyafanyia kazi; na

vii. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa Sera na kuziwasilisha kwa Kamati ya Uwezeshaji ya Wizara.

### 3.3.2. Dawati la Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania la Mkoa

Ofisi ya Katibu Tawala Msaidizi Sehemu ya Uchumi na Uzalishaji ndiyo itaratibu Dawati la Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania la Mkoa kwa niaba ya Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) kutokana na nafasi yake katika kuwezesha masuala ya uchumi na uzalishaji. Katibu Tawala Msaidizi Sehemu ya Uchumi na Uzalishaji atakuwa mratibu wa uwezeshaji kiuchumi wa mkoa na atawajibika kwa RAS/RCC katika masuala ya uwezeshaji wananchi kiuchumi. Kwa maana hiyo mtaalam atawasilisha kwa RCC taarifa ya utekelezaji na baada ya kuidhinishwa na kamati hiyo ataiwasilisha kwa Baraza kwa niaba ya RCC.

#### 3.3.2.1 Majukumu ya Dawati la Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania la Mkoa

i. Kuratibu, kusimamia na kufuatilia shughuli za uwezeshaji zinazofanywa katika Halmashauri zote mkoani kwa niaba ya RCC;

ii. Kutafsiri na kusimamia utekelezaji wa Sera na Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Mkakati wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi katika mkoa;

iii. Kukusanya taarifa na tafiti mbalimbali na kushauri mkoa kuhusu masuala ya uwezeshaji wananchi kiuchumi na ushiriki wa watanzania katika uwekezaji;

iv. Kuandaa bajeti ya uwezeshaji kila mwaka na kuhakikisha inaingia katika bajeti ya mkoa;

v. Kubuni na kutafuta vyanzo vya raslimali kwa ajili ya shughuli za uwezeshaji katika mkoa wake;

vi. Kuratibu na kuhamasisha uanzishwaji na uendelezaji wa vikundi vya

kiuchumi kama SACCOS, VICOBA na vingine vinavyosajiliwa toka ngazi ya wilaya hadi taifa;

vii. Kuhakisha kuwa mkoa na kila Halmashauri mkoani inatoa kipaumbele (preferential treatment) kwa watanzania katika utoaji wa zabuni zake;

viii. Kufuatilia taarifa za uwezeshaji toka Halmashauri zilizopo mkoani na kuzijumuisha katika kuandaa taarifa ya mkoa;

ix. Kuwasilisha taarifa ya Mkoa ya Utekelezaji wa Uwezeshaji kwa RCC; na

x. Kuwasilisha taarifa ya utekelezaji kwa RCC na baada ya kukubaliwa itumwe kwa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na TAMISEMI.

### 3.3.3. Dawati la Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania la Halmashauri

Kila Halmashauri inawajibika kuteua Ofisi ya Maendeleo ya Jamii kuratibu Dawati la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushiriki wa Watanzania chini ya Mkurugenzi wa Halmashauri. Dawati litafanya kazi kwa niaba ya Kamati ya Uwezeshaji ya Halmashauri. Mtaalam kiongozi katika ofisi hii atakuwa mratibu wa uwezeshaji kiuchumi wa Halmashauri na atawajibika kwa Kamati ya Uwezeshaji ya Halmashauri (Kamati ya Ujenzi, Uchumi na Mazingira) katika masuala ya uwezeshaji wananchi kiuchumi. Kwa maana hiyo atawasilisha taarifa ya utekelezaji kwa kamati na baada ya kuidhinishwa na kamati hiyo atawasilisha kwa Mratibu wa Uwezeshaji Mkoa na nakala kwa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

#### 3.3.3.1 Majukumu ya Dawati la Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania la Halmashauri

i. Kusimamia na kufuatilia shughuli za uwezeshaji zinazofanywa katika kata na vijiji/mitaa katika Halmashauri;

ii. Kutafsiri na kusimamia utekelezaji wa Sera na Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Mkakati wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi katika Halmashauri;

iii. Kukusanya taarifa na tafiti mbalimbali na kumshauri Mkurugenzi wa Halmashauri katika masuala ya uwezeshaji kiuchumi;

iv. Kuhakikisha fedha za uendeshaji zinatengwa katika bajeti kila mwaka kwa ajili ya masuala ya uwezeshaji;

v. Kuhakikisha kuwa Halmashauri inahusisha suala la hifadhi ya Mazingira na mabadiliko ya Tabia Nchi katika Mipango ya Maendeleo ya Wilaya ili kuboresha mazingira ambayo ni muhimu katika suala zima la uzalishaji mazao ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi;

vi. Kubuni na kutafuta vyanzo vya rasilimali kwa ajili ya shughuli za uwezeshaji katika Halmashauri yake;

vii. Kuratibu na kuhamasisha uanzishwaji na uendelezaji wa vikundi vya kiuchumi kama SACCOS, VICOBA na vingine vinavyosajiliwa na kutambuliwa toka ngazi ya wilaya hadi taifa;

viii. Kuwasilisha taarifa ya utekelezaji kwa Kamati ya Uwezeshaji ya Halmashauri na baada ya kuidhinishwa itumwe kwa Mratibu wa Uwezeshaji Mkoa na nakala kwa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;

ix. Kuhamasisha vikundi vya kijamii na kiuchumi kujisajili/kujirasimisha na kufanya uzalishaji wenye viwango vya TBS, TFDA na kupata nembo ya utambuzi wa bidhaa (msimbomilia (Barcode));

x. Kuandaa taarifa ya maendeleo ya vyama vya ushirika hasa SACCOS na vikundi vya kiuchumi kama VICOBA vilivyopo katika Halmashauri;

xi. Kubuni fursa mbalimbali za uwekezaji katika Halmashauri;

xii. Kufuatilia upatikanaji wa masoko ya bidhaa za kiuchumi;na

xiii. Kushauri namna ya uboreshaji wa vituo vidogovidogo vya kibiashara, hususan, katika vijiji na Mamlaka za Miji Midogo.

### 3.3.4. Dawati la Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania la Kata

Halmashauri inawajibika kuteua Mtaalam (Afisa Maendeleo ya Jamii na kama hayupo ateuliwe Afisa Ugani) katika kata zote kuratibu Dawati la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushiriki wa Watanzania katika kata. Dawati litafanya kazi kwa niaba ya Kamati ya Maendeleo ya Kata na mtaalam katika dawati hili ataitwa Mratibu wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi wa Kata.

#### 3.3.4.1 Majukumu ya Dawati la Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania la Kata

i. Kusimamia na kufuatilia shughuli za uwezeshaji zinazofanywa katika vijiji/mitaa;

ii. Kutafsiri na kusimamia utekelezaji wa Sera na Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Mkakati wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi katika kata;

iii. Kusambaza taarifa na matokeo ya tafiti mbalimbali kuhusu Uwezeshaji wananchi kiuchumi katika Kata;

iv. Kubuni na kutafuta vyanzo vya mapato kwa ajili ya shughuli za uwezeshaji katika kata yake;

v. Kuhamasisha uanzishwaji na uendelezaji wa vikundi vya kiuchumi kama SACCOS, VICOBA na vinginevyo vinavyosajiliwa na kutambuliwa toka ngazi ya wilaya hadi taifa katika kata yake;

vi. Kufuatilia taarifa za uwezeshaji toka vijiji/mitaa na kuzijumuisha katika kuandaa taarifa ya kata;

vii. Kuhamasisha vikundi vya kijamii na kiuchumi kujisajili/kujirasimisha na kufanya uzalishaji wenye viwango vya TBS, TFDA na kupata nembo ya utambuzi wa bidhaa (msimbomilia (Bar code)); na

viii. Kuwasilisha taarifa ya utekelezaji kwa Kamati ya Maendeleo ya Kata na baada ya kuidhinishwa itumwe kwa Mratibu wa Uwezeshaji wa Halmashauri.

### 3.3.5. Dawati la Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania Ngazi ya Kijiji/Mtaa

Uratibu wa Uwezeshaji katika ngazi ya Kijiji/Mtaa utafanywa na Mtaalam wa Serikali kama Afisa Ugani akishirikiana na Halmashauri ya kijiji/mtaa kwa niaba ya mkutano mkuu wa kijiji/Mtaa. Kama kijiji hakina Afisa Ugani, Afisa Mtendaji wa Kijiji atakuwa Mratibu wa Uwezeshaji katika kijiji. Vivyo hivyo katika Mtaa Afisa Mtendaji ndiye Mratibu wa Uwezeshaji wa Mtaa.

#### 3.3.5.1. Majukumu ya Dawati la Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania Ngazi ya Kijiji/Mtaa

i. Kufuatilia na kuhakikisha kuwa miradi ya uwezeshaji toka Halmashauri ya wilaya inawafikia wananchi wake;

ii. Kuhakikisha kuwa wanawake na vijana katika kijiji/mtaa wanashiriki katika shughuli za kiuchumi ipasavyo na kufikiwa na mifuko yao ya maendeleo ya kiuchumi iliyopo katika Halmashauri ya wilaya;

iii. Kushawishi, kuhamasisha na kuhakikisha kuwa Halmashauri ya kijiji/mtaa husika inatenga maeneo maalum kutegemeana na mahitaji ya sasa na ya baadaye kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi zikiwemo biashara ndogondogo za vijana na wanawake;

iv. Kuhamasisha na kuwezesha maendeleo ya vikundi vya kiuchumi kama SACCOS na VICOBA katika kijiji/mtaa husika;

v. Kuelekeza na kufuatilia utekelezaji wa malengo ya uzalishaji mali kwa kila mwananchi aliyefikia umri wa miaka kumi na nane (18);

vi. Kudadisi, kubuni na kushirikisha kamati ya uwezeshaji ya kijiji/mtaa kukusu namna ya uongezaji thamani na upatikanaji masoko kwa mazao ya wakulima, wafugaji na wazalishaji mali wengine katika kijiji/mtaa;

vii. Kuhimiza familia kuanzisha miradi kama ya Ufugaji Nyuki katika maeneo yao ili kuongeza kipato katika jamii na kuhifadhi mazingira; na

viii. Kuandaa taarifa ya Uwezeshaji ya kijiji/mtaa na kuwasilisha kwa Kamati ya Uwezeshaji ya Kijiji/Mtaa, kwa Mkutano Mkuu wa Kijiji/Mtaa na baadaye katika ngazi ya Kata;

# SURA YA NNE

## 4.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KATIKA UTEKELEZAJI WA MWONGOZO

Ili kutelekeza mwongozo huu kwa mafanikio ni muhimu wadau wote wanaotekeleza masuala ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi wazingatie mambo muhimu yafuatayo katika shughuli zao za kila siku:-

**i. Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo Iliyopo katika Utekelezaji wa Kazi za Kila Siku**

Katika kutekeleza majukumu ya kila siku ya Uwezeshaji kila Kiongozi, Kamati, Madawati ya Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania na Wananchi kwa jumla wanatakiwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali iliyopo.

**ii. Kujenga Uelewa wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na masuala yote ya Uwezeshaji kwa Watumishi na Watendaji katika Ngazi husika**

Viongozi wa Taasisi za Umma, Mikoa, Halmashauri, Kata, na Vijiji/Mitaa), Sekta Binafsi, Wanataaluma, Asasi za Kiraia, na Wadau mbalimbali watambue kuwa wanalo jukumu kubwa la kujenga, kuelimisha na kutaasisisha masuala ya uwezeshaji kwa watumishi, watendaji na Taasisi zao na katika jamii kwa jumla.

**iii. Ushirikiano na Wadau Mbalimbali katika kutekeleza Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi**

Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi imeainisha nguzo tisa za utekelezaji ambazo zimeonyeshwa katika Sura ya Pili ya Mwongozo huu. Nguzo hizi hazitekelezwi na Taasisi moja tu, wala si jukumu la Taasisi ratibu pekee bali ni jukumu la jamii nzima. Hivyo, wadau mbalimbali na jamii kwa jumla wanapaswa kushirikiana katika jukumu la Uwezeshaji katika ngazi zote.

**iv. Kuepuka Mgongano wa Masilahi**

Watendaji wote wa ngazi za utekelezaji wa Mwongozo huu wanapaswa kuepuka migongano ya kimaslahi katika kutekeleza miradi, programu, zabuni na majukumu mbalimbali ambayo yanalenga kumwezesha Mwananchi kiuchumi.

# SURA YA TANO

## 5.0 UFUATILIAJI NA TATHMINI YA UWEZESHAJI

Kila taasisi husika, itahakikisha kuwa kazi ya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya Uwezeshaji katika sekta na maeneo husika inafanyika. Ili kufanikisha jukumu hili kila sekta itatakiwa ipange na kutenga bajeti ya kufuatilia na kutathmini majukumu ya Uwezeshaji. Zoezi hili litafanikisha upatikanaji wa taarifa za utekelezaji na kufahamu mafanikio ya sekta husika katika kuinua uchumi wa wananchi katika kushiriki na kumiliki uchumi wa nchi yao.

Ufuatiliaji na tathmini uzingatie utekelezaji wa kila kipengele cha jukumu kilichoainishwa katika ngazi husika ya kiutendaji na utekelezaji katika Mwongozo huu. Hii itaenda sambamba na kufuatilia na kutathmini miradi, programu na uwekezaji mbalimbali unaofanyika katika maeneo ya kiutendaji. Taarifa zitokanazo na ufuatiliaji na tathmini zitatoa taswira ya Serikali ya utekelezaji wa shughuli za Uwezeshaji kwa wananchi wake.

Imeandaliwa na:
Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC)
12 Barabara ya Kivukoni
S.L.P. 1734 Dar-Es-Salaam
Simu: +255 22 2137362
Simu/Nukushi: +255 22 2125596
Barua Pepe : neec@uwezeshaji.go.tz
Tovuti : www.uwezeshaji.go.tz